

KANUNI ZA BUNGE

(Toleo la 2004)

ZIMETUNGWA KWA MUJIBU WA MARA YA 89(I) YA KATIBA YA JAMHURI YA MUUNGANO

SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

1. Kanuni hizi ziiitwe Kanuni za Bunge, toleo la mwaka 2003.

2.-(1) Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vinginevyo.

Jina

Ufafanuzi

"Bendera" maana yake ni Bendera ya Bunge inayotajwa katika Kanuni za 121,122 na 123.

"Gazeti" maana yake ni Gazeti rasmi la Serikali ya Jamhuri ya Muungano linaloitwa Gazeti la Serikali au *The Tanzania Gazette*;

"Hoja ya Kamati" maana yake ni hoja inayotokana na majadiliano ya Kamati yoyote ya Bunge;

"Hoja ya Mbunge" maana yake ni hoja inayotolewa na Mbunge asiyekuwa Waziri;

"Kamati" maana yake ni Kamati yoyote ya Bunge iliyoundwa kwa Mujibu wa Kanuni hizi;

"Kamati inayohusika" maana yake ni Kamati itakayopewa kazi fulani kwa mujibu wa Kanuni ya 88(9);

"Kamati ya Bunge Zima" maana yake ni Kikao cha Wabunge wote wanapokuwa wamekaa kama Kamati ya Bunge, badala ya kukaa kama Bunge lenyewe. Lakini wakati wa Kamati ya Bunge Zima inaposhughulikia Makadirio ya Matumizi ya Fedha za Serikali, itaitwa "Kamati ya Matumizi";

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977, pamoja na marekebisho yake yote;

"Katibu" maana yake ni Katibu wa Bunge, na ni pamoja na Naibu Katibu, Katibu Msaidizi na Mtumishi mwingine yeyote wa Bunge aliyeidhinishwa kutekeleza kazi yoyote ya Katibu wa Bunge;

"Kikao cha Bunge" maana yake ni kikao cha siku moja kinachoanza kwa kusomwa Dua na kumalizika kwa kuahirisha Bunge hadi siku inayofuata, au siku nyingine ya baadaye;

"Kitabu cha Maamuzi" maana yake ni kumbukumbu iliyotajwa katika Kanuni ya 14(3), inayohusu maamuzi mbalimbali ya Bunge na maamuzi ya Spika kuhusu suala lolote la utaratibu Bungeni;

"Kitabu cha Shughuli" maana yake ni kumbukumbu ya kudumu inayowekwa na Katibu kwa mujibu wa Kanuni ya 14(1)(d);

"Maisha ya Bunge" maana yake ni ule muda wote unaoanzia tarehe ambapo Bunge jipya limeitishwa kukutana mara ya kwanza baada ya Uchaguzi Mkuu na kuishia tarehe ya kuvunjwa kwa Bunge hilo; "Mbunge" maana yake ni Mjumbe wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

"Mkutano wa Bunge" maana yake ni mfululizo wa vikao, kuanzia kikao cha kwanza hadi kufikia wakati ambapo shughuli zote zilizopangwa zitakuwa zimemalizika;

"Mgeni" maana yake ni mtu yeyote ambaye si Rais, Mbunge, Katibu au Mtumishi mwingine yeyote ambaye hatekelezi kazi rasmi zinazohusu Bunge; isipokuwa kwamba mtu yeyote ambaye si Mbunge au mtumishi wa Bunge hatahesabiwa kama mgeni atakapokuwa anafanya kazi zinazohusu Bunge au Shughuli za Bunge, na kwa kiasi kinachomwezesha kufanya kazi hizo tu;

"Rais" maana yake ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na ni pamoja na mtu mwingine yeyote ambaye kwa wakati fulani unaohusika atakuwa anatekeleza kazi za Rais kwa Mujibu wa Katiba;

"Spika" maana yake ni Spika wa Bunge. Isipokuwa kwamba Naibu Spika, Mwenyekiti wa Bunge au Mbunge mwingine yeyote anapokuwa amekalia Kiti cha Spika, katika Kikao chochote cha Bunge, au anapokuwa akitelekeza shughuli yoyote ambayo ni kazi ya Spika, atakuwa na madaraka yote ambayo yamekabidhiwa kwa Spika kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Mwenyekiti" maana yake ni Mbunge aliyechaguliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, kuongoza Shughuli za Bunge wakati Spika na Naibu Spika wote hawapo. Neno "Mwenyekiti" pia litatumika kwa Spika, Naibu Spika au Mbunge mwingine anayehusika wakati anapokuwa anaongoza Kamati ya Bunge Zima;

"Siwa" maana yake ni Rungu la dhahabu linaloturnika kama kielelezo cha Mamlaka ya Spika ambalo hubebwa na Mpambe wa Bunge aliyetajwa katika Kanuni ya 16 ya Kanuni hizi, akimtangulia Spika wakati anapoingia na kutoka kwenye Ukumbi wa Bunge kabla na baada ya kila Kikao cha Bunge; na vile vile hufunikwa lisionekane wakati Bunge linapokaa kama Kamati ya Bunge Zima;

"Taarifa Rasmi" maana yake ni Taarifa ya majadiliano ya Bunge iliyotajwa kwa mujibu wa Kanuni hizi;

"Vikao vya Bunge" maana yake ni pamoja na Vikao vya Karnati zake;

"Waziri" ni pamoja na Naibu Waziri na pia Waziri Mkuu.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya Katiba, Kanuni hizi zitatumika katika uendeshaji wa Shughuli zote za Bunge.